***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania….!***

Leo tumejumuika pamoja hapa Songea kwa ajili ya maadhimisho ya kitaifa ya Siku ya UKIMWI Duniani. Namshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kunialika kuwa Mgeni rasmi kwenye Maadhimisho haya. Pamoja na shukrani hizo, nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kanali Ahmed Abbas Ahmed, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma na uongozi wa Mkoa na wananchi wote kwa mapokezi na maandalizi mazuri ya maadhimisho haya.

***Ndugu Viongozi na Wananchi,***

Dhima ya maadhimisho haya ni kutukumbusha kuhusu wajibu wetu katika mapambano dhidi ya janga la UKIMWI na kutuwezesha kutafakari, kuweka na kutekeleza mikakati endelevu ya kinga dhidi ya maambukizi mapya ya VVU; kutokomeza unyanyapaa na kumaliza vifo vitokanavyo na UKIMWI. Siku hii pia inatuwezesha kuwakumbuka wenzetu waliopoteza maisha yao kutokana na UKIMWI pamoja na kuwafariji waathirika wa janga hili wakiwemo watoto yatima ambao wazazi wao walifariki kutokana na UKIMWI. Maadhimisho haya yamekuwa yakifanyika kitaifa na katika mikoa mbalimbali kila mwaka, tangu mwaka 2001. Maadhimisho ya mwaka huu yanabeba Kaulimbiu isemayo **"Chagua Njia Sahihi, Tokomeza UKIMWI"**, ambayo inatoa msukumo kwa kila mmoja wetu kushiriki kikamilifu katika kupambana na maambukizi mapya, huduma kwa walioathirika na matunzo kwa yatima na watoto waliozaliwa na maambukizi. Imethibitika kuwa jitihada za kupambana na UKIMWI zinafanikiwa zaidi pale ambapo kuna ushiriki mzuri wa jamii, vyama na mashirika yasiyo ya kiserikali, kutokuwepo kwa ubaguzi na uwepo wa rasilimali za kutosha ili kuwezesha mapambano.

***Ndugu Wananchi,***

Tangu mapambano dhidi ya UKIMWI yalipoanza takriban miongo minne iliyopita, mfanikio makubwa yamepatikana. Kwa mfano, matokeo ya utafiti wa viashiria vya VVU na UKIMWI uliofanyika mwaka 2022/23, yanaonesha kuwa maambukizi mapya miongoni mwa watu wazima wenye umri kuanzia miaka 15 ni watu 60,000 kwa mwaka. Aidha, kiwango cha ushamiri wa VVU kitaifa ni 4.4% ambapo jumla ya watu 1,548,000 wanaishi na VVU.

Kiwango cha ushamiri wa VVU kwa wenye umri kuanzia miaka 15 na zaidi kwa upande wa Tanzania Bara ni 4.5% na 0.4% kwa upande wa Zanzibar. Viwango vya ushamiri kwa mikoa ya Tanzania Bara vinaanzia 1.7% (Kigoma) hadi 12.7% (Njombe). Mikoa mitatu ya Mbeya, Iringa na Njombe ina viwango vya ushamiri zaidi ya 9% ambayo ni mara mbili ya kiwango cha Kitaifa.

***Ndugu Wananchi,***

Malengo ya mapambano dhidi ya UKIMWI duniani ifikapo mwaka 2025 ni 95-95-95 (yaani, 95% ya Watu wote wanaoishi na VVU kupima na kujua Afya zao; 95% ya wote Waliopima na Kuwa na maambukizi ya VVU kuanza kutumia Dawa; na 95% ya Wanaotumia Dawa

wawe wamefubaza VVU). Katika utafiti uliofanyika nchini imebainika kuwa katika watu wenye umri wa miaka 15 na zaidi, wanaoishi na maambukizi ya VVU:

- Katika kundi la kwanza, 82.7% wanajua hali zao za maambukizi (ikilinganishwa na 61% miaka mitano iliyopita, sawa na ongezeko la 22%);
- Katika kundi la pili, 97.9% ya wanaojua hali zao za maambukizi wameanza kutumia dawa za kufubaza makali ya VVU (ikilinganishwa na 94% miaka mitano iliyopita, sawa na ongezeko la 4%); na
- Katika kundi la tatu, 94.3% ya watu wanaotumia dawa za kufubaza makali ya VVU, wamefubaza (ikilinganishwa na 87% miaka mitano iliyopita, sawa na ongezeko la 7%*)*.

Matokeo haya ni hatua nzuri na yenye kuleta matumaini katika kuelekea lengo la kutokomeza UKIMWI ifikapo 2030. Matokeo ya utafiti huo, yanatupa ushahidi wa jinsi afua mbalimbali zinavyofanya kazi, na vikwazo au changamoto zilizopo. Hivyo, ninaiagiza TACAIDS kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu kuchakata kikamilifu taarifa za utafiti huo ili kuwezesha maeneo yenye changamoto kufanyiwa kazi kwa umakini.

***Ndugu Wananchi,***

Pamoja na mafanikio makubwa katika huduma za kinga, tiba na matunzo, ningependa kurudia tena kusisitiza mambo muhimu yafuatayo katika kukabiliana na UKIMWI.

**Jambo la kwanza,** ni kuhusu tatizo sugu la unyanyapaa na ubaguzi. Mtazamo hasi uliopo juu ya walioathirika, huchangia kurudisha nyuma jitihada za kupambana na UKIMWI. Hali hii huwafanya wahitaji kushindwa kupata huduma kwa kuonekana kuwa hawastahili na hivyo kutengwa. Unyanyapaa hupelekea woga unaoathiri upimaji kwa hiari na upatikanaji wa huduma nyingine kama za unasihi pamoja na ARV kwa wale wanaoishi na VVU. Katika hili, naomba tuungane pamoja kutoa elimu kuanzia ngazi ya mtu binafsi, familia na jamii kwa ujumla ili kupata uelewa wa VVU na UKIMWI kwa kina na kuondoa mitazamo hasi.

**Jambo la pili,** ni maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Hali ya maambukizi mapya inaonekana kuchochewa zaidi na mazingira na tabia hatarishi hususan ulevi uliopindukia, ngono zembe, kuwa na wapenzi wengi na matumizi ya dawa za kulevya. Kwa kiasi fulani, baadhi ya mila na desturi zetu pia zimechangia maambukizi mapya ya VVU. Naendelea kutoa rai kwa wananchi kuzingatia maudhui ya elimu inayotolewa kupitia kampeni mbalimbali kwa ajili ya kubadili tabia, kuachana na mila zinazoweza kuwa vichocheo vya maambukizi na kuendelea kujikinga na maambukizi mapya ya Virusi Vya UKIMWI. Kasi ya maambukizi katika kundi la vijana bado inaonekana kuwa kubwa. Takwimu za hali ya UKIMWI nchini zinaonesha kuwa kundi la vijana na hasa wa kike liko kwenye hatari zaidi ya kupata maambukizi mapya ya VVU. Natoa rai kwa TACAIDS kushirikiana na Wizara za Kisekta, wadau na jamii kwa ujumla kuweka mkazo katika kudhibiti mazingira yanayochochea maambukizi. Aidha, natoa wito kwa vijana kujitambua, kujithamini na kutunza maisha yao kwa kujikinga na maambukizi mapya ya VVU. Kwa vijana ambao tayari wanaishi na VVU waendelee kutumia dawa za ARV kwa usahihi ili kufubaza makali ya virusi na kuimarisha afya zao.

***Ndugu Wananchi,***

Mafanikio yaliyopo katika mapambano dhidi ya UKIMWI yamechangiwa kwa kiasi kikubwa na ushirikiano mzuri uliopo baina ya Serikali na wadau mbalimbali ikiwemo sekta binafsi. Kwa namna ya pekee natoa shukrani za Serikali kwa Mfuko wa Dunia (Global Fund), Mfuko wa Dharura wa Rais wa Marekani wa UKIMWI (PEPFAR) na Mashirika ya Umoja wa Mataifa kwa kuendelea kutuunga mkono kwenye utekelezaji wa afua mbalimbali za VVU na UKIMWI. Kwa namna ya kipekee, napenda kutumia fursa ya maadhimisho haya kuwashukuru kwa dhati *Global Alliance for Vaccine and Iniatives (GAVI)* kwa ufadhili wa magari 96 na pikipiki 300, vyenye thamani ya billioni 8 kwa ajili ya kuimarisha huduma za chanjo kwenye halmashauri zetu. Msaada huu utachangia kwa kiasi kikubwa kuboresha huduma za chanjo na kuwakinga watoto dhidi ya magonjwa yanayozuilika. Nawapongeza na kuwashukuru wadau wote kwa kuunga mkono jitihada za Serikali.

***Ndugu Wananchi,***

Kwa kumalizia, nawapongeza kwa dhati waandaaji wa maadhimisho haya na wananchi wa mkoa wa Ruvuma kwa kufanikisha maadhimisho haya ya Siku ya UKIMWI Duniani. Mwitikio na ushiriki wenu katika maadhimisho haya ni wa kupigiwa mfano. Baada ya kusema hayo, sasa niko tayari kuzindua sehemu ya kwanza ya Mpango Kazi wa Uendelevu wa mwitikio wa UKIMWI *(Part I of the Development of the HIV Response Sustainability Roadmap)*. Mpango kazi huo utaweza uandaaji wa Mkakati wa utekelezaji utakaoanza kuandaliwa hivi karibuni.

***"Chagua Njia Sahihi, Tokomeza UKIMWI"***

**Asanteni sana Kwa kunisikiliza!**